## Maswali

1. Mbona wakuu wa Wayahudi walikasirikia Stefano?
2. Wakuu wa Wayahudi walilipa watu wafanye nini?
3. Stefano alipelekwa kwa hakimu wa Hekalu. Stefano aliwakumbusha nini?
4. Stefano alisema Waisraeli walifanyaje manabii wa Mungu?
5. Stefano alisema Wayahudi walifanyaje Yesu?
6. Wakuu wa Wayahudi na watu wengine walifanya nini Stefano aliposema hivyo?
7. Stefano aliona maono gani yaliyompa nguvu
8. Stefano aliomba nini kwa Yesu?
9. Wakuu wa Wayahudi na watu wengine walifanyaje Stefano?
10. Nini itafanyika kwa Stefano Yesu atakapokuja hapa duniani?

## Majibu

1. Kwa sababu alifundisha juu ya Yesu na watu wengi wakawa Wakristo.
2. Waseme uongo juu ya Stefano kwamba amezungumza maovu juu ya Mungu na juu ya Hekalu.
3. Ibrahimu, Yusufu na nduguze, Musa na Waisraeli, Waisraeli kukataa Mungu kama Mfalme na kumuasi.
4. Wayahudi walikuwa wametesa na kuua manabii.
5. Wayahudi walikuwa wameua Yesu Kristo, Mwana wa Mungu.
6. Walipiga kelele kwa ghadhabu, wakamburura Stefano nje ya mji na kumpiga kwa mawe.
7. Aliona Mbingu imefunguliwa na Yesu amesimama mkono wa kuume Mungu.
8. Aliomba kwamba Yesu asiwasabulie hiyo dhambi.
9. Walimpiga Stefano kwa mawe na akafa.
10. Yesu atafufua Stefano kutoka kwa wafu. Stefano atasaidia Yesu kutawala ulimwengu.

**SHULE YA JUMAPILI YA CBM**

**Awamu ya 2 Mwaka wa 2**

# 91 Stefano anapigwa kwa mawe

### Kwa Biblia

Matendo ya Mitume mlango wa 6 na 7:51 – 60

### Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu huwa karibu na wale wampendao wakati wako kwa shida. Yesu atafufua wafu atakapokuja

### Somo

Stefano alikuwa bado kijana. Alikuwa Mkristo. Stefano alijazwa Roho Mtakatifu. Alifanya miujiza mingi katika jina la Yesu. Stefano na Wakristo wengine sita walijaguliwa ili wawashugulikie wajane na watu maskini. Stefano alisaidia kwa kulinda pesa zilizotolewa na Wakristo ili kuwasaidia maskini. Tena Stefano alihubiri Habari Njema kuhusu Yesu Kristo na Ufalme wa Mungu.

Watu wengi walisikiliza Stefano alipokuwa akiwambia habari ya Yesu. Watu wengi waliamini na wakabatizwa. Wakuu wa Wayahudi hawakupenda Wakristo. Walimchukia Stefano kwa sababu alifundisha watu wengi kuwa Wakristo. Wakuu wa Wayahudi walitaka kuzuia Stefano asifundishe juu ya Yesu. Wakuu wa Wayahudi walituma watu wabishane na Stefano. Walitaka kumfanya aonekane kuwa ni mjinga.

Mungu alikuwa anasaidia Stefano. Stefano alijua neno la Mungu vizuri sana. Watu hao hawangeweza kuwa kinyume na maneno yake ya hekima. Wakuu wa Wayahudi walikasirika sana. Waliamua kuua Stefano.

Wakuu wa Wayahudi walilipa watu kusema uongo juu ya Stefano. Hao watu walisema maneno maovu juu ya Stefano. Walisema Stefano alikuwa amezungumza vibaya juu ya Mungu na juu ya Hekalu takatifu. Maneno haya mabaya yalifanya watu wakasirikie Stefano. Stefano alipelekwa Hekaluni kuhukumiwa.



Stefano alisimama mbele ya hakimu wa Hekalu. Watu waovu walizungumza uongo juu yake. Halafu Stefano aliulizwa ajibu huo uongo juu yake. Stefano hakuwakasirikia wale watu waliosema uongo juu yake. Stefano alijawa na upendo kutoka kwa Mungu. Waliokuwa hapo wakati wa hukumu walimwangalia na kusikiliza Stefano. Uso wake ulijawa na upendo hata akaonekana kama malaika.

Kwanza Stefano alizungumza juu ya mashujaa wa Biblia. Aliwakumbusha juu ya Ibrahimu. Aliacha nyumbani kwao na marafiki huko Uru. Alienda kuishi kwa nchi yenye Mungu alimwambia aende.

Stefano aliwakumbusha juu ya Yusufu. Aliuzwa Misri na nduguze. Stefano aliwakumbusha juu ya Musa. Aliwaongoza Waisraeli kutoka Misri utumwani. Aliwaongoza kupitia jangwani. Wakati wote, Waisraeli walinukunikia Musa.

Stefano aliwakumbusha kwamba kila mara Waisraeli waliasi Mungu na kuabudu sanamu. Walimkataa Mungu kama Mfalme wao.

Stefano aliwakumbusha kwamba alikuwa akiwapa wafalme. Alituma manabii wengi kuwafunza. Lakini Waisraeli waliwatesa na kuwaua manabii. Walikataa kusikiliza maneno ya Mungu. Aliambia waliokuwa wakimuhukumu. "Nyinyi ni kama Waisraeli baba zenu. Waliwatesa na kuua manabii. Mlimtesa na kuua Yesu Kristo Mwana wa Mungu."



Waliposikia hayo, watu waliokuwa hapo Hekaluni, walipiga kelele kwa ghadhabu. Stefano aliangalia juu na akaona maono, akaona Yesu akampa nguvu. Aliwambia, "Angalia, ninaona Mbingu imefunguliwa na Mwana wa Adamu amesimama mkono wa kuume wa Mungu." Wakuu wa Wayahudi na watu wengine walipiga kelele wakisema, "Unakufuru! Unakufuru!"

Wakuu wa Wayahudi walikimbia kwa Stefano. Wakamburura mpaka nje ya mji. Waliweka nguo zao chini ya miguu ya kijana aliyeitwa Sauli. Halafu wakachukua mawe na wakaanza kupiga Stefano. Stefano alianguka chini. Waliendelea kumtupia mawe.

Stefano alipokuwa akifa aliomba Yesu, "Bwana Yesu, wasamehe." Alipomaliza kuomba hivyo, alikufa.

Stefano alikuwa Mkristo wa kwanza kwa Wakristo wengi kufa kwa ajili ya Yesu. Hii hadithi ni ya uchungu lakini itakuwa na mwisho mzuri. Stefano alipenda Bwana Yesu sana. Hivi karibuni Yesu atarudi hapa duniani. Yesu atafufua Stefano kutoka kwa wafu. Stefano atasaidia Yesu kutawala ulimwengu.